# PROFILE YA IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI




*Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama*

## 1.0 Utangulizi

Idara ya Utawala na Utumishi idara inayoshughulikia masuala yote ya Utawala na Kiutumishi katika kuhakikisha watumishi wa Halmashauri ya Wilaya wanakuwa na ari ya kufanya kazi na kutoa huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Mkalama.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama Mhandisi Godfrey Sanga.*

Idara hii ina maafisa Utumishi wanne, Mkuu wa Idara mmoja na wasaidizi wake watatu:-

1. Khashim S. Lugome- 0764509602
2. Stella J. Mawa- 0756820847
3. Richard C. Laizer- 0627648454
4. Godfrey E. Mnubi- 0756966358



*Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ndugu Khashim Lugome.*

## 2.0 Idadi ya watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama

Halmashauri ya wilaya ya mkalama inajumla ya idara ya Idara/Vitengo 19 watumishi 1347 wa Idara na vitengo tofauti kama ilivyo katika mchanganuo ufuatao**:-**

## 2.1 Mkurugenzi na Wakuu wa Idara/Vitengo

2.1.0 Jedwali Mkurugenzi na kuonyesha Wakuu wa Idara/Vitengo waliopo katika H/W ya Mkalama

| Idara/Kitengo | Mkuu wa Idara/Kitengo | Mawasiliano ya simu |
|---|---|---|
| Mkurugenzi mtendaji (W) | Eng, Godfrey T. Sanga | 0714772300/0783668043 |
| Utawala na Utumishi | Khashimu S.Lugome | 0686101346/0764509602 |
| Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji | Ally Shemdolwa | 0769568847 |
| Afya | Deogratias B.Masini | 0714460159 |
| Fedha na Biashara | | |
| Elimu msingi | Chacha J. Kehogo | 0752915560/0717781990 |
| Elimu Sekondari | Fredy A. Kimeme | 0784986294 |
| Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | Cuthbert G. Mwinuka | 0755680126/0784893510 |
| Mifugo na Uvuvi | Elias E. Mbwambo | 0789111720 |
| Maendeleo ya jamii, Ustawi wa Jamaii na Vijana | Elias M. Mollel | 0783534834 |
| Maji | Edwin J. Ntungilwege | 0787763246 |
| Usafi na Mazingira | Amon Ben Kiwanga | 0755025812/0785638336 |
| Ujenzi | Paskazia S. Tibalinda | 0718265523 |
| Ardhi na Maliasili | John M. Langas | 0784408250/0653349917 |
| Sheria | Lilian A. Kasanga | 0766019409/0683979807 |
| Ukaguzi wa ndani | Albins | 0784-395994/0755-776490 |

| | | |
|---|---|---|
| | Hayahaimo | |
| Ugavi | Sebastian M. Kindi | 0759798484 |
| Uchaguzi | Abdallah J. Njelu | 0759759823/0783947776 |
| Teknolojia Habari na Mawasiliano | John M. Malasa | 0784376511/0766174801 |
| Ufugaji nyuki | | |

## 3.0 Idadi ya watumishi kwa kila Idara/Kitengo

3.1.0 Jedwali kuonyesha Idadi ya Watumishi katika Idara/Vitengo

| Na. | Idara/Kitengo | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Utawala na Utumishi | 102 |
| 2 | Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji | 5 |
| 3 | Afya | 199 |
| 4 | Fedha na Biashara | 13 |
| 5 | Elimu msingi | 678 |
| 6 | Elimu Sekondari | 267 |
| 7 | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 20 |
| 8 | Mifugo na Uvuvi | 22 |
| 9 | Maendeleo ya jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana | 7 |
| 10 | Maji | 6 |
| 11 | Usafi na Mazingira | 1 |
| 12 | Ujenzi | 5 |
| 13 | Ardhi na Maliasili | 3 |
| 14 | Sheria | 1 |
| 15 | Ukaguzi wa ndani | 2 |
| 16 | Ufugaji Nyuki | |
| 17 | Ugavi | 2 |
| 18 | Uchaguzi | 1 |

| | | |
|---|---|---|
| 19 | Teknolojia Habari na Mawasiliano | 2 |
| | **JUMLA** | |

## 4.0 Majukumu ya Idara ya Utawala na Utumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama

- Kusimamia nidhamu ya Watumishi na kuhakikisha Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma zinafuatwa
- Kuandaa Bajeti ya Mishahara ya Watumishi kwa kila mwaka wa fedha.
- Kuhakikisha Watumishi wanaostahili kupanda Vyeo Watumishi wanapata haki yao.
- Kuajiri Watumishi wa kada zinazoruhusiwa kwa mujibu wa miongozo na kuomba kibali cha Ajira kwa Watumishi wanaotahiniwa na Sekretarieti.
- Kuwapa na kuwapeleka watumishi katika mafunzo pamoja na kuwaendeleza kitaaluma ili kuwaongezea hamasa na ufanisi katika kazi.
- Kuhakikisha watumishi wanakuwa katika mazingira salama ya kufanyia kazi.
- Kusimamia mfumo wa wazi wa mapitio na tathmini ya upimaji utendaji kazi (OPRAS)
- Kuimarisha mahusiano ya watumishi kazini (Employee Relations).

## 5.0 Malengo ya Idara ya Utawala kwa mwaka 2017/2018

1. Kuwapandisha vyeo watumishi **412** na kuwathibitisha kazini watumishi **30** wa kada mbalimbali ifikapo Juni 2018.
2. Kuajiri watumishi **625** wa kada mbalimbali ifikapo Juni 2018
3. Kutunza kumbukumbu za watumishi waliopo, waliofariki, wanaostaafu, wanaohama, walioacha kazi na kushughulikia maslahi mbalimbali ya watumishi.
4. Kusimamia na kuratibu shughuli za kujenga uwezo wa kutoa huduma za Halmashauri kwa kusimamia mafunzo ya watumishi**,** ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi, utunzaji wa vifaa na usafi wa mazingira nje na ndani ya ofisi.
5. Kumalizia Ujenzi wa jengo **1** la Ofisi ya Halmashauri na kujenga nyumba **4** za watumishi ifikapo Juni 2018
6. Kuratibu vikao **14** vya Menejimenti ya Timu ya Halmashauri (C.M.T.) ifikapo Juni 2018
7. Kuratibu vikao **5** vya Kamati ya Huduma za Jamii ifikapo Juni 2018.
8. Kuratibu vikao **5** vya Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi na Mazingira ifikapo Juni 2018
9. Kuratibu Vikao **13** vya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ifikapo Juni 2018.
10. Kuratibu vikao **4** vya vya Mkutano wa Halmashauri ifikapo Juni 2018.
11. Kuratibu vikao **3** vya bodi ya Ajira ya Halmashauri ifikapo Juni 2018
12. Kuratibu vikao **3** vya kamati ya Uadilifu ifikapo Juni 2018.
13. Kuratibu vikao **3** vya kamati ya Kudhibiti Ukimwi mahala pa kazi ifikapo Juni 2018.
14. Kusimamia na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi, kutoa ufafanuzi kwa watumishi juu ya sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.
15. Kuratibu ufanyikaji wa vikao ngazi ya Kata na Vijiji.
16. Kuratibu Sherehe za Kitaifa.



*Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama*

## 6.0 Mafanikio ya Idara ya Utawala na Utumishi.

- Hadi kufikia Februari 2018 Idara imefanikiwa kupunguza tatizo la watumishi kwa asilimia kubwa (zaidi ya 50%) kwa kuomba na kupata vibali vya ajira za watumishi wapya kwa kada mbalimbali.
- Idara imefanikiwa kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Makao makuu kwa kuhakikisha jengo la Halmashauri ya Wilaya linakamilika kwa wakati pia kuwapatia Vitendea kazi kama viti, meza, Kompyuta watumishi wa waliopo vituoni.
- Idara imefanikiwa kuhakiki Vyeti vya Kidato cha nne kwa Watumishi wote walioko kazini na zoezi hili linaendelea kadiri tunapopata Watumishi wapya.

- Idara imefanikiwa kuratibu ufanyikaji wa vikao vya kisheria ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.
- Idara imefanikiwa kutoa Mafunzo ya PlanRep na FFARS kwa watumishi wa Idara mbalimbali kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.
- Idara imefanikiwa kutoa mafunzo ya awali (Orientation) kwa watumishi wapya 38 wa Idara ya Utawala na Utumishi kwa mawaka wa fedha 2017/2018.
- Idara imefanikiwa kuwadhibitisha kazini watumishi 27 wa Idara mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- Idara imefanikiwa kuajiri watumishi 125 wa kada mbalimbali kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.